

## Mchezo Wa Kamali.

Katika jamii ya Tanzania, mchezo wa kamali sio kitu kipyaa lakini hata hivyo ni tatizo linalokua katika jamii hii ya leo, kitu chochote tufanyacho twahitaji kwanza kuangalia maandiko ili kuona kama yale tufanyayo yapo katika neno (Kol. 3:17) ndilo lengo la somo hili Je, kamali ni tendo jema kwa Mkristo kushiriki? Biblia ikitisema jambo fulani ni baya basi inabidi tusijihushe nalo ili tuweze kukubaliwa na Mungu.

Nina maana gani ninaposema mchezo wa kamali? Kwa kifupi ni mchezo wenyenafasi ama hatari ya pesa kwa kutumaini kupata zaidi, kamali ni pamoja na hatari ya kupoteza mali, nafasi ya kushinda kumiliki mali ya watu wengine lakini ni wazi kuwa haiwezekani kushinda watu wote mpaka mmojawapo apoteze.

Mchezo wa kamali upo katika namna mbalimbali katika jamii yetu mchezo wa kadi, kurusha shilingi, kuzungusha mashine, mchezo wa mpira, loto, bingo na mingine mingi . Mtu ambaye hasomi maneno la Mungu anaweza kufikili kama hiyo ni burudani kuchezea hela lakini tunapaswa kufikili na kufahamunini mungu anatueleza kwenye maneno yake hivyo tuweze kuangalia misingi ya Biblia.

1. Maandiko yanatufundisha njia tatu za kuhamisha mali na pesa kutoka mtu mmoja hadi mwingine mtu aweza kufanya kazi na kupata ujira (Lk. 10:7; Mat. 10:10; Efe. 4: 28) mtu aweza kuuza vitu, mali au vifaa na kupata au ujira ( Lk.6:30,43,35; 10:33-35; mdo. 20:35) kuwa wakristo ni watu wanaoendesha maisha yao kwa kufuata jinsi mamlaka ya Mungu inavyowaelekeza tunaweza kuona kwamba kamali imezuiwa katika maisha ya Mkristo, hakuna popote utakapoona Paulo akicheza kamali ili apate pesa ya kufanya kazi yake kwa sababu kamali haipo sehemu yoyote kwenye Biblia.

2. Kanuni ya pili ambayo inaelezwa kwenye Biblia ni kuwa, kamali inaungani sha watu wawili wakishindana ili wachukue Pesa ya mtu mwingine wote wacheza kamali wanakuwa wanataka, kuchukua pesa ya mtu mwingine lakini wao hawapendi kumchangia mwenzao. Wote wacheza kamali wanatamani kushinda pesa ya wenzao lakini wao hawapendi kupoteza paesa zao. Hali hii ya kuchezza kamali, ipo inaleta msuguano katika msingi wa moyo wa Mkristo kama inavyoelezwa na Yesu katika Math.7:12. Je, ungelipenda wewe udanganywe kwa pesa yako mwenyewe? Kama sivyo kwa nini uwadanganye wengine?

Hivyo mchezo wa kamali unawatendea wengine kinyume na ambavyo mtu mhusika angependa ataendewe anataka pesa yao lakini hataki kupoteza ya kwake kwa moyo huo ni dhambi, ubinagsi, uchoyo na wivu.

3. Tatizo la tatu ni uhasama katika kufanyakazi, imefundishwa wazi katika maneno ya Mungu kwamba tufanye kazi tutumie mikono yetu, tutoe jasho(Mdo. 20:35; 2 Thes.3-8-12, Ef. 4:28). Kuchezza kamali ni kwenda kinyume na mpango wa Mungu, kwa kutaka vyaa bweelele kwa jasho la wengine (kula kulala).

4. Tatizo la mwisho ni husuda au wivu Mungu anatutaka tufanye kazi ili tuweze kupata kipato kwa ajili ya maisha ya kila siku kwa familia 1Tim. 5:8; Gal. 6:10; Kutafuta/ kutengeneza hela ili tuishi ni tofauti na kuishi li utengeneze fedha.

Mungu anatuonya mara nyingi kote kwenye historia ya Binadamu kuwa tuondoe mawazo yetu tamaa ya kutaka vitu na tamaa ya kupata utajiri (Math. 6:19-21; Lk.12: 15-21; Ef. 5:3; Kol. 3:1-5; 1Yoh. 2 15-17) Paulo anayataja haya kama mawazo ya utajiri kupenda fedha, kutegemea utajiri unaopita (1 Tim. 6:9,10, 17) .

Kamali ni kinyume cha kila kazi ya Mungu leo. Mcheza kamali sio mtu mtakatifu ila ni mtu mbinafsi anayependa kunyang'anya. Pesa toka kwa watu wengine wala hajali utaratibu wa Math. 7:12. Tujipatie hela na vitu vingine kwa njia sahihi ambazo tunafanya kazi.